

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA



Mtaa wa Kingalu
S.L.P 845 MOROGORO
Simu: 023-2614302
Nukushi: 023-2614478
Barua Pepe:
rbcmorogoro@pccb.go.tz
Wavuti: www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA KUPITIA VYOMBO VYA HABARI

Juni 11, 2020

POLISI KINARA WA MAPAMBANO YA RUSHWA
AMNASISHA MWINGINE TAKUKURU

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Morogoro leo JUNI 11, 2020 imemfikisha mbele ya Mahakama ya Hakimu wa Wilaya ya Kilosa **Ramadhani B. Arufan Kaluona** Mkazi wa Kijiji cha Simbalambende kilichopo katika Kata ya Ruaha Wilayani Kilosa kwa kosa la kumhonga fedha kiasi cha **Shilingi Laki Nne [400,000/=]** Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai wa Wilaya ya Kipolisi ya Ruhembe **ASP Onesphory Emmanuel Lesiyo** kitendo ambacho ni kinyume na kifungu cha 15(1) (b) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa **Na. 11/2007**.

Fedha hizo alizitoa ikiwa ni kishawishi cha kuiachilia pikipiki yake yenye usajili wa **Na. MC 406 BVY** iliyokamatwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za ubebaji wa bidhaa za magendo.

Akisomewa mashtaka yake katika shauri Na. **125/2020** mbele ya Hakimu wa Wilaya ya Kilosa Mheshimiwa **Timothy Lyon** mtoa Rushwa huyo **Ramadhani Arufan Kaluona** amekana mashtaka hayo na yuko nje kwa dhamana hadi tarehe 23/07/2020 shauri litakapokuja tena kwa ajili ya usikilizwaji wa awali.

Awali; mapema mwezi Februari, 2020 Mkuu huyo wa upelelezi **ASP Onesphory Emmanuel Lesiyo** aliwezesha pia kukamatwa kwa mshtakiwa mwingine katika shauri la

Jinai Na. **36/2020** lililoko mbele ya Mahakama hiyo **Bw. William Bony Chiotola** kwa kosa la hongo chini ya kifungu cha 15 (1) (b) cha sheria tajwa. Mshtakiwa huyo alikamatwa akitoa hongo ya **Shilingi Laki Tatu na Eflu Arobaini [Shs. 340,000/=]** kama kishawishi cha kuacha kuwachukulia hatua ndugu zake kwa tuhuma za kukutwa na madawa ya kulevya.

Ushupavu wa kutoa taarifa za vitendo vya Rushwa uliofanywa na **ASP Onesphory Emmanuel** ni kitendo cha kizalendo cha kupigiwa mfano kwa kila mtumishi wa umma mwenye dhamana yoyote katika Mkoa wa Morogoro na jamii yote kwa ujumla.

Kitendo hicho kinachagiza mapambano dhidi ya adui mbya Rushwa na kuondoa fikra potofu za kihalifu kwa baadhi ya wanajamii ambao wanaamini kuwa wana nguvu ya kufanya vitendo vya kihalifu kwa kuwa wana uwezo wa kuwahonga maafisa wenye dhamana.

Wengine waliofikishwa mbele ya Mahakama hiyo leo kwa makosa ya kupokea hongo chini ya kifungu 15(1) (a) cha Sheria hiyo ni **Kisalanzo Mganga** ambaye ni Mtendaji wa Kata ya Leshata wilayani Gairo kwa kupokea hongo ya **Shilingi Laki Moja [Shs. 100,000/=]** kama kishawishi cha kutomchukulia hatua mtoa taarifa anayedaiwa kuruhusu ng'ombe waliokamatwa kinyume na taratibu na **Juma Hassan Shelukindo** ambaye ni Mlinzi wa Mahakama ya Mwanzo Idibo - Gairo kwa kupokea hongo ya Shilingi Eflu Arobaini [**Shs. 40,000/=**] kama kishawishi cha kutoa dhamana kwa mlalamikaji aliyeshikiliwa kwa madai ya kutishia kwa maneno.

TAKUKURU inaendelea kutoa WITO kwa wananchi wote wa Morogoro kushiriki kikamilifu katika mapambano dhidi ya Rushwa.

Imetolewa na:

Janeth Machulya,

MKUU WA TAKUKURU (M),

MOROGORO